

1. Onyesha shamirisho, kitendo, kipozi na kitumizi katika sentensi ifuatayo  
**“Kidadi alimbebea Dadi mzigo kwa mkokoteni”**
2. Tunga sentensi yenyе kikundi tenzi chenye muundo ufuatayo:  
**Kitenzi kisaidizi, kitenzi kikuu, nomino**
3. Tunga sentensi tatu kuonyesha matumizi matatau ya kiambishi :li”
4. Tunga sentensi yenyе muundo ufuatao:  
KN(N)+KT(T+E)+KN(N)+KT(T+E)
5. Bainisha kiima na hagizo katika sentensi ifuatayo:  
**Wakulima wote walivuna mazao yao kwa furaha**
6. Andika visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari  
**Shaibu yake alishikwa na kisunzi**
7. Akifisha sentensi ifuatayo kubainisha dhana tatu tofauti:  
**Julius Kipkemboi mwanawe Ruto na Kibagenge  
walikiletea kijiji chao sifa**
8. Ainisha maneno yaliyopigiwa mistari  
**Naam, ameleta machache**
9. Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo  
**Kiharusi chake kimemtia hofu**
10. Tunga sentensi ukitumia kivumishi cha nomino.

- 11.** Sahihisha sentensi hii  
**Waya yangu imekatika**
- 12.** Tambua mzizi katika neno **msahaulifu**
- 13.** (i) Fafanua maana ya mofimu huru  
(ii) Toa mifano miwili ya mofimu huru.
- 14.** Neno **chuo** lina maana ya shule inayotoa mafunzo muhimu ya kazi Fulani. Tunga sentensi mbili kubainisha matumizi mengine mawili ya neno hili.
- 15.** Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo:
- Ngao alimpigia husda mpira**
- 16.** Unda nomino kutokana na
- (i) Zingua
  - (ii) Fumbua
  - (iii) Tosa
  - (iv) Zindua
- 17.** Tunga sentensi mbili kuonyesha maana tofauti za maneno yafuatayo
- (i) Rudi
  - (ii) Chuma
- 18.** (i) Eleza maana ya sentensi ya masharti  
(iii) Tunga sentensi moja ya masharti
- 19.** Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi mawili tofauti ya kistari kifupi.
- 20.** Nukta pacha hutumiwa katika kuorodhesha. Onyesha matumizi mengine matatu ya alama hii

21. (i) Eleza maana ya kirai  
(I) Ainisha virai vilivyopigiwa mstari
- Samani hizi zimeundwa na maseremara wenye ujuzi mkubwa**
22. Huku ukitoa mfano, eleza maana ya **sentensi ambatano**
23. Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya: koga na konge
24. Andika visawe viwili vya nahau: **Enda mrاما**